

# Maswali

1. Wapelelezi wangapi walienda Yeriko?
2. Waliishi kwa nyumba ya nani?
3. Ni nani alisikia kukuja kwa wapelelezi?
4. Ni ujumbe gani mfalme alitumia Rahabu?
5. Rahabu alijibu mfalme nini?
6. Rahabu aliwaficha wapi wapelelezi?
7. Wapelelezi waliahidi Rahabu nini?
8. Wapelelezi walimwambia afunge nini kwa dirisha lake?
9. Wapelelezi walitokaje Yeriko?
10. Wapelelzi walijificha kwa siku ngapi mlimani?

# Majibu

1. Wapelelezi wawili walienda Yeriko.
2. Waliishi kwa nyumba ya Rahabu.
3. Mfalme alisikia kwamba wapelelezi walikuwa wamekuja.
4. Ujumbe wa mfalme ultaka Rahabu awatoe wale wapelelezi.
5. Rahabu alimwambia mfalme kwamba walikuwa wameondoka.
6. Rahabu alificha wapelelezi darini.
7. Wapelelezi waliahidi kuokoa Rahabu na jamaa yake.
8. Wapelelezi waliambia Rahabu afunge kamba nyekundu kwa dirisha lake.
9. Wapelelezi walitoka kwa kuteremshwa kwa kamba.
10. Wapelelezi walijificha kwa siku tatu mlimani.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM



**Awamu ya 1 Mwaka wa 1**

## **19 Rahabu na wapelelezi**

### **Marejeo**

Yoshua 2

### **Kiini cha somo**


Kuonyesha maana ya kuwa na imani kwa Mungu

### **Maneno maalum**

1. Jangwani siku 40 + Yoshua kiongozi mpya + wapelelezi Yeriko
2. Rahabu + Mfalme wa Yeriko + wapelelezi watolewe + Rahabu asema + fuata wapelelezi
3. Rahabu aficha wapelelezi + Rahabu aamini Mungu + ahadi ya wapelelezi + kamba nyekundu
4. Wapelelezi wahepa + kamba dirishani + ficha siku 3 + okoka + ambia Yoshua

**19.1** Wana wa Israeli walisafiri jangwani kwa mika 40. Mungu aliwaambia wataenda mpaka nchi ya ahadi. Musa alikufa na Yoshua akawa kiongozi mpya. Yoshua kwa siri alituma wapelelezi wawili. "Enda muone hiyo nchi," Yoshua alisema, "zaidi sana Yeriko."

**19.2** Wapelelezi walienda Yeriko na kukaa kwa mwanamke aitwaye Rahabu.



Mfalme wa Yeriko aliarifiwa kwa kukuja kwao. "Kuna watu wamekuja. Wana wa Israeli kupeleleza nchi yetu," mfalme aliwaambia.

Mfalme alitumana kwa Rahabu. Watu wa mfalme walisema, "Walete hao watu wenye wamekuja kwa nyumba yako usiku huu ni wapelelezi."

"Ndio," Rahabu alisema, "Walikuja kwangu lakini sijui walikotoka. Wakati lango la mji lilipokuwa likifungwa na usiku kuingia, walitoka. Wafuate upesi mtawashika." Watu wa mfalme walifuata upesi na mlango wa mji ukafungwa nyuma yao.

**19.3** Lakini alikuwa amewaficha kwa dari ya nyumba yake, chini ya mabua ya kitani aliyokuwa akikausha (mabua ni mmea unaotumiwa kwa kutengeneza nguo).

Watu wa mfalme walipoondoka, Rahabu akapanda darini. Akawaambia wapelelezi, "Ninajua Bwana amepeana hii nchi kwa wana wa Israeli. Watu wote wanamuogopa. Tumesikia vile Mungu alimkaushia maji kwa Bahari ya Shamu. Nimekuwa mzuri kwenu," Rahabu alisema. "Niahidi kwamba hata ninyi mtakuwa wazuri kwangu mtakapochukuwa mji wa Yeriko. Niahidi kwamba mtaokoa mimi na jamaa yangu."

Wapelelezi waliahidi Rahabu. Wapelelezi waliambia Rahabu, "Tutakaposhambulia mji huu, funga hii kamba nyekundu kwa dirisha lako ili mtu ye yote wa jamii yako hataumizwa."

**19.4** Rahabu aliwateremsha kwa kamba kupitia dirishani mpaka nje kwa sababu nyumba yake ilijengwa kwa ukuta wa mji. "Enda milimani," aliwaambia, "mkajifice huko siku tatu mpaka watu wa mfalme warudi nanyi mtapona."

Kwa hivyo Rahabu aliwaruhusu waende. Walienda na kumwambia Yoshua yote yaliyotendeka.

